JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2008 CERTIFIED

TAARIFA KWA UMMA

UFAHAMU KUHUSU MATUMIZI SAHIHI NA SALAMA YA MITANDAO YA KOMPYUTA NA INTANETI

1. UTANGULIZI

Kitengo cha dharura cha kuitikia matukio ya usalama kwenye mitandao nchini ***(Tanzania Computer Emergency Response Team- TZ-CERT)*** kimepewa jukumu la kitaifa la kuratibu matukio ya usalama katika mitandao ya kompyuta na intaneti, kwa kushirikiana na vyombo vingine husika vya kikanda na kimataifa, katika kusimamia matukio ya usalama mitandaoni.

TZ-CERT ilianzishwa kwa sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya 2010, kifungu namba 124. Kifungu namba 5(1) cha kanuni za Mawasiliano ya kielektroniki na Posta (Timu ya kuitikia matukio ya dharura ya usalama mtandaoni) zilizotolewa Desemba 2011, kilielekeza uanzishwaji wa Timu ya kuitikia matukio ya dharura ya usalama mtandaoni ijulikanayo kwa kifupi **TZ-CERT**, ndani ya mfumo wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Huduma za TZ-CERT zilizinduliwa rasmi tarehe 17 mwezi Mei mwaka 2015.

Majukumu makuu ya TZ-CERT kisheria ni kuwa kiungo cha kitaifa nchini na kwa nchi za nje kwa masuala yote yanaohusiana na usalama mtandaoni. Katika kutimiza wajibu huo, TZ-CERT:

1. Inatoa ushauri wa kitaalamu wa kukabiliana na matukio ya kiusalama yanayotokea na kwa lengo la kuzuia madhara,

2. Inafanya uchambuzi wa taarifa za matukio ya usalama wa mtandao kutoka vyanzo mbalimbali, vya kimataifa na kitaifa, na kutumia matokeo ya uchambuzi huo kuongeza usalama wa matumizi ya kompyuta na mtandao wa intaneti,

3. Kutoa mwongozo wa kitaalamu kwa umma na wadau katika maeneo ambayo yameonekana kuwa na madhaifu,

4. Uhamasisha, elimisha na kujenga uwezo wa masuala ya usalama wa mitandao kwa umma, serikali na wadau kutoka sekta mbalimbali.

5. Hufanya tathimini ya udhaifu wa mifumo ya kompyuta *ya* mitandao ya wadau wake.

Ikumbukwe kwa sasa Tanzania kuna watumiaji wa mtandao wanaokadiriwa kufikia milioni kumi na nane (**18 milioni**) kutokea milioni tano (**5 milioni**) katika mwaka 2011.

Kutokana na uzoefu uliopatikana kwa muda wa mwaka mmoja toka TZ-CERT ianze rasmi kutoa huduma zake, TCRA imebaini, pamoja na mambo mengine ukosefu wa taarifa muhimu za matumizi sahihi na salama ya mitandao kumechangia kuwepo kwa matukio ambayo yangeweza kuepukika.

2. Kwa nini kuongeza ufahamu wa matumizi bora ya Mtandao?

Kuongeza ufahamu kumekuja wakati muafaka baada ya TZ-CERT kubaini changamoto nyingi na aina mbalimbali za matatizo yaliyotokea wanayokutana nayo wanchi wengi ambayo yametokana na kuwa na ufahamu mdogo wa jinsi ya kujilinda ukiwa unatumia huduma zilizopo katika mitandaoni kompyuta ma intaneti, kulinda taarifa zao pamoja na matumizi sahihi ya mtandao kwa ujumla wake kama yanavyo tolewa na watoa huduma.

3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA UTUMIAPO HUDUMA ZA INTANETI/MITANDAO

i. Kuwa makini na taarifa za binafsi unazoziweka kwenye mitandao wa jamii,

ii. Ukisaidiwa kuanzisha akaunti za mtandao wa kijamii, hakikisha unabadilisha neno la siri lilotumika mara moja; neno lako la siri ni siri yako usimshirikishe mtu mwingine,

Tunza neno lako la siri unalotumia katika huduma zako za kwenye mtandao, mfano barua pepe, miamala ya kibenki.

iii. Usijibu jumbe unazopokea kwenye akaunti yako ya barua pepe au ujumbe mfupi wa simu unaoulizia taarifa au unaokutaka kuhakiki taarifa zako binafsi za akaunti za huduma mbalimbali kwenye mtandao wa intaneti bila kuhakiki uhalali wa taarifa husika,

iv. Usijibu ujumbe wowote wa barua pepe unaokueleza kuwa umeshinda bahati nasibu bila kuhakiki uhalali wa barua pepe husika,

v. Usifungue kiambatisho au kubofya kiungo (link) unayotumiwa na mtu usiye mjua kabla ya kuhakikisha uhalali wa barua pepe husika.

vi. Tumia programu za kompyuta za wakati na hakikisha kompyuta au kifaa chako cha kielektroniki zinatumia program zakujikinga na virusi hatarishi.

vii. Tumia muda kujielimisha kwa kusoma taarifa mbalimbali zinazohusiana na hudama za mtandao wa intaneti unazotumia.

Ili kujiepusha kukiuka sheria mbalimbali za mawasiliano ya mtandao, unashauriwa kuzingatia yafuatayo:

i. Usitunge na kusambaza ujumbe wa maudhi, uzushi au uchochezi,

ii. Usiendelee kusambaza ujumbe wa chuki, maudhi au uchochezi unaopokea kutoka kwa mtu mwingine. Badala yake ufute mara uupokeapo au toa taarifa,

iii. Usitembelee tovuti au blogu za ponografia/ngono,

iv. Usitengeneze akunti za mitandao ama kwa lengo la kufanya utapeli, ulaghai au kwa kutumia taarifa zisizo zako,

v. Tunza kwa usalama vifaa vya kielektroniki unavyotumia kuhifadhi kumbukumbu zako na usitumie vifaa hivi kwenye kompyuta za umma.

4. FAIDA ZA HUDUMA ZA MITANDAO:

i. Hurahisisha mawasiliano.
ii. Hupunguza gharama.
iii. Huongeza ufanisi.
iv. Huokoa muda.

5. TAARIFA ZAIDI NA MAWASILIANO

- Pata taarifa zaidi kutoka kwenye tovuti ya TZ-CERT kwa anuani ifwatayo: www.tzcert.go.tz.

  Tovuti hii pia inatoa nafasi ya kutuma na kutoa taarifa za matukio mbali mbali kwa wataalamu wa TZ-CERT unapo hitaji msaada .

- Kwa kutoa taarifa za tukio ili kupata msaada tumia anwani ya barua pepe ifwatayo: incidents@tzcert.go.tz au info@tzcert.go.tz

- Pia unaweza kuwasiliana kupata taarifa muhumi na kutoa maoni au kuuliza maswali kwa kutumia akaunti za mitandao ya kijamii zifwatazo:

  https://www.facebook.com/Tz-Cert

  https://twitter.com/tz_cert

  https://www.instagram.com/

- Kwa mawasiliano ya simu piga: 022 2412 039 au 022 2199760-9

Imetolewa na:

MKURUGENZI MKUU
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)
Mawasiliano Towers
20 Barabara ya Sam Nujoma
S.L.P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA
20 Septemba 2017